







# Matarajio na matokeo:
## Vipaumbele, utendaji na siasa nchini Tanzania

## 1. Utangulizi

Siku 500 zimepita tangu Rais John Magufuli aingie madarakani na kuteua timu ya watendaji wakuu katika sekta mbalimbali. Kipindi hiki kinatosha kuwapa wananchi mwenendo wa vitendo vya serikali na kuona jinsi ambavyo aina ya uongozi huu unavyoyagusa maisha yao ya kila siku.

Muhtasari huu umebeba maoni ya wananchi juu ya masuala ya kisiasa. Kwa mtazamo wao, ni tatizo gani kuu linaloikabili nchi kwa sasa? Je, tatizo hilo limebadilika ukilinganisha na miaka iliyopita? Je, wananchi wanauonaje utendaji wa viongozi wao, akiwemo Rais? Na je, kuna mabadiliko yoyote katika kukubalika kwa vyama mbalimbali vya siasa katika kipindi cha miaka michache iliyopita?

Takwimu za muhtasari huu zinatoka *Sauti za Wananchi* iliyopo Twaweza. *Sauti za Wananchi* ni utafiti wa kwanza barani Afrika wenye uwakilishi wa kitaifa unaotumia simu za mikononi. Utafiti huu una uwakilishi wa Tanzania Bara pekee. Taarifa kuhusu mbinu za utafiti huu zinapatikana kupitia www.twaweza.org/sauti. Takwimu za muhtasari huu zilikusanywa kutoka kwa wahojiwa 1,805 katika awamu ya 18 ya kundi la pili la *Sauti za Wananchi*. Takwimu hizi zilikusanywa kati ya tarehe 31 Machi na tarehe 17 Aprili mwaka 2017.

Matokeo muhimu ni:

- Wananchi wametaja umasikini/hali ngumu ya kiuchumi kama tatizo kuu linaloikabili Tanzania kwa sasa.
- Idadi ya wananchi wanaotaja upungufu wa chakula kama tatizo kubwa imeongezeka.
- Idadi ya wananchi wanaotaja rushwa kuwa tatizo kubwa imepungua.
- Tofauti na miaka iliyopita, ni wananchi wachache wanaokubali utendaji wa viongozi waliowachagua mwaka 2017.
- Asilimia 71 wanaukubali utendaji wa Rais Magufuli.
- Asilimia 84 ya wananchi wanasema huenda watapiga kura kwenye uchaguzi mkuu mwaka 2020.
- Asilimia 63 wapo karibu zaidi na CCM kuliko vyama vingine.
- Idadi ya wananchi wanaofungamana na Chadema imeshuka tangu mwaka 2013.

Imetolewa na Twaweza East Africa

P. O. Box 38342, Dar es Salaam, Tanzania.
t: +255 22 266 4301, | e: info@twaweza.org |
www.twaweza.org/sauti



Twaweza
ni sisi


## 2. Mambo tisa kuhusu maoni ya wananchi juu ya masuala ya kisiasa

### Jambo la 1: Wananchi wanataja umasikini/uchumi duni kama tatizo kubwa linaloikabili Tanzania

Umasikini (asilimia 60), upungufu wa chakula (asilimia 57) na afya (asilimia 40) ndio changamoto kuu zinazowakabili wananchi kwa sasa.

Idadi ya wananchi waliotaja huduma za umma (afya, elimu na maji) kama matatizo makubwa matatu yanayoikabili nchi imepungua ikilinganishwa na miaka iliyopita.

**Kielelezo cha 1: Kwa mtazamo wako, ni matatizo gani makubwa matatu yanayoikabili Tanzania kwa sasa? (asilimia ya waliotaja tatizo husika katika mlolongo wa tatu bora)**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*: Kundi la 1 utafiti wa awali (Oktoba-Desemba 2012), Awamu ya 10 (Oktoba 2013) na Awamu ya 24 (Septemba 2014), na Kundi la 2 Awamu ya 1 (Agosti-Septemba 2015) na Awamu ya 18 (Aprili 2017)

## Jambo la 2: Idadi ya wananchi wanaotaja upungufu wa chakula kama tatizo kubwa imeongezeka huku wanaotaja rushwa ikipungua

Idadi kubwa ya wananchi (asilimia 57) imetaja upungufu wa chakula kama suala linalostahili kipaumbele kati ya masuala matatu makubwa yanayoikabili Tanzania kwa kipindi huki. Hii imeongezeka ikilinganishwa na asilimia 7 hadi 20 ya miaka iliyopita.

Idadi ya wananchi wanaotaja rushwa au uongozi kama moja ya matatizo makubwa imepungua kwa kiwango kikubwa: kutoka asilimia 24 hadi 30 mwaka 2012-2015 mpaka asilimia 10 mwaka huu.

**Kielelezo cha 2: Kwa mtazamo wako, yapi ni matatizo makubwa matatu yanayoikabili Tanzania kwa sasa? (asilimia ya waliotaja suala kwenye tatu bora; masuala yaliyochaguliwa)**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*: Kundi la 1 utafiti wa awali (Oktoba-Desemba 2012), Awamu ya 10 (Oktoba 2013) na Awamu ya 24 (Septemba 2014), na Kundi la 2 Awamu ya 1 (Agosti-Septemba 2015) na Awamu ya 18 (Aprili 2017)

## Jambo la 3: Asilimia 84 wanasema watapiga kura katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020

Asilimia 84 ya wananchi wanasema watapiga kura katika uchaguzi mkuu utakaofanyika mwaka 2020. Hata hivyo, asilimia 8 wamesema huenda hawatopiga kura, na idadi kama hiyo (asilimia 8) hawajaamua kama watapiga kura au la.

Ieleweke kuwa ni jambo la kawaida kwa baadhi ya wananchi wanaosema watapiga kura kutofanya hivyo ifikapo siku ya uchaguzi. Utafiti wa *Sauti za Wananchi* wa mwaka 2015 ulionesha kwamba, kati ya asilimia 99 waliosema watapiga kura mwka huo, ni asilimia 67[1] tu waliojitokeza kufanya hivyo.

**Kielelezo cha 3: Je, utapiga kura katika uchaguzi mkuu ujao wa mwaka 2020?**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, awamu ya 18 (Aprili 2017)

## Jambo la 4: Viwango vya kukubalika kwa wenyeviti wa vijiji/mitaa, kata, madiwani na wabunge vimeshuka katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

Mwaka 2012, asilimia 88 waliukubali utendaji wa mwenyekiti wao wa kijiji au mtaa. Hata hivyo, ni asilimia 66 tu walio na maoni kama hayo mwaka huu. Vilevile, kati ya mwaka 2012 na 2017, idadi ya wananchi waliokubali utendaji wa madiwani wao imeshuka kutoka asilimia 85 mpaka asilimia 59, na idadi ya waliokubali utendaji wa wabunge wao imeshuka kutoka asilimia 79 hadi asilimia 58.

1 Angalia http://www.twaweza.org/uploads/files/PolPoll-EN-FINAL.pdf

**Kielelezo cha 4: Asilimia ya wanaokubali utendaji wa viongozi waliowachagua tangu walipoingia madarakani**





**Chanzo cha takwimu:** Utafiti wa *Sauti za wananchi*, Kundi la 1 utafiti wa awali (Oktoba-Desemba 2012), Awamu ya 10 (Oktoba 2013) na Awamu ya 24 (Septemba 2014), na Kundi la 2 Utafiti wa Awali (Julai-Agosti 2015), Awamu 11 (Juni 2016) na Awamu ya 18 (Aprili 2017)

## Jambo la 5: Wananchi saba kati ya kumi wanaukubali utendaji wa Rais Magufuli

Asilimia 71 ya wananchi wanaukubali utendaji wa Rais John Pombe Magufuli. Hii ni pungufu kutoka asilimia 96 ya waliokubali utendaji wake mwaka 2016.

Kati ya mwaka 2012 na 2015, viwango vya kukubalika kwa Rais Jakaya Kikwete vilikuwa kati ya asilimia 81 na asilimia 87.

**Kielelezo cha 5: Asilimia ya wanaokubali utendaji wa Rais Magufuli tangu alipoingia madarakani**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*: Kundi la 1 Utafiti wa Awali (Oktoba-Desemba 2012), Awamu ya 10 (Oktoba 2013) na Awamu ya 24 (Septemba 2014), na Kundi la 2 Utafiti wa Awali (Julai-Agosti 2015), Awamu ya 11 (Juni 2016) na Awamu ya 18 (Aprili 2017)

Wastani wa viwango vya kukubalika kwa marais wa Afrika kama vilivyorekodiwa katika tafiti 128 za utafiti wa *Afrobarometer* tangu mwaka 1999 ni asilimia 63[2].

Ni kawaida kwa viwango vya kukubalika kwa marais kushuka baada ya kipindi cha mwanzo cha kuingia madarakani. Utafiti wa *Pew* kwa mfano, unaonesha viwango vya kukubalika kwa marais tisa kati ya kumi na moja wa mwisho nchini Marekani vikishuka[3]. (haijaoneshwa kwenye jedwali)

## Jambo la 6: Rais Magufuli anakubalika zaidi miongoni mwa vikundi vya wazee na wenye elimu isiyozidi ya msingi


Pengo kubwa la kukubalika kwa Rais Magufuli linaonekana katika makundi ya rika mbalimbali: asilimia 68 wenye umri chini ya miaka 30 wanamkubali Rais ikilinganishwa na asilimia 82 wenye umri zaidi ya miaka 50. Elimu nayo inachangia; asilimia 75 ya wananchi wasiokuwa na elimu au wenye elimu ya msingi tu wanamkubali Rais wakati asilimia 63 ya wale wenye elimu ya sekondari au elimu ya juu ndio wanaomkubali Rais. Pia kiwango cha kukubalika ni kikubwa miongoni mwa wananchi masikini (asilimia 75) kuliko matajiri (asilimia 66).

2 Angalia http://afrobarometer.org

3 http://www.pewresearch.org/fact-tank/2016/01/12/presidential-job-approval-ratings-from-ike-to-obama/

Hakuna tofauti kubwa katika viwango vya kukubalika kwa Rais kati ya wanawake (asilimia 73) na wanaume (asilimia 70), au kati ya wakazi wa vijijini (asilimia 72) na mjini (asilimia 70).

**Kielelezo cha 6: Ni kwa kiasi gani unaukubali utendaji wa Rais tangu alipoingia madarakani?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 (Aprili 2017)

## Jambo la 7: Asilimia 63 wanasema wapo karibu zaidi na CCM kuliko chama kingine chochote

Asilimia 63 ya wananchi wanasema wapo karibu zaidi na chama cha CCM kuliko chama kingine chochote. Asilimia 17 wapo karibu na chama cha Chadema, na idadi ndogo wapo karibu na chama cha CUF (asilimia 1), ACT- Wazalendo (asilimia 1) na NCCR Mageuzi (asilimia 1). Asilimia 17 wanasema hawana ukaribu na chama chochote.

**Kielelezo cha 7: Je, ni chama gani unachoona upo karibu nacho zaidi? (Taja kama kipo)**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*, Awamu ya 18 (Aprili 2017)

## Jambo la 8: Kukubalika kwa Chadema kumeshuka tangu mwaka 2013

Ukilinganisha na asilimia 32 ya wananchi waliosema wapo karibu na chama cha Chadema mwaka 2013, ni asilimia 17 wanaosema hivyo mwaka huu. Wakati huo huo, uungwaji mkono CUF Tanzania Bara umeshuka kutoka asilimia 4 hadi asilimia 1.

Hata hivyo, asilimia 17 wanasema hawana ukaribu na chama chochote, ikilinganishwa na chini ya asilimia 5 waliosema hivyo miaka iliyopita.

**Kielelezo cha 8: Upo karibu na chama gani cha siasa, taja kama kipo?**





**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa *Sauti za Wananchi*: utafiti wa awali (Oktoba-Desemba 2012), Kundi la 1 Awamu ya 10 (Oktoba 2013) na Awamu ya 24 (Septemba 2014), Kundi la 2 Awamu ya 1 (Agosti-Septemba 2015) na Awamu ya 18 (Aprili 2017)

## Jambo la 9: CCM inakubalika zaidi miongoni mwa wazee, wenye kiwango cha chini cha elimu, masikini, wanawake na wakazi wa vijijini

CCM inakubalika zaidi miongoni mwa wazee (asilimia 80), ukilinganisha na asilimia 55 ya vijana. Wanawake (asilimia 68) wanaikubali CCM kuliko wanaume (asilimia 58), maeneo ya vijijini (asilimia 66) kuliko maeneo ya mijini (asilimia 57), na wananchi masikini (asilimia 69) kuliko matajiri (asilimia 53). Wananchi wenye elimu ya sekondari, elimu ya ufundi au elimu ya juu wanaikubali CCM kwa asilimia 46.

**Kielelezo cha 9: Chama gani cha siasa upo karibu nacho taja kama kipo?**




**Chanzo cha Takwimu:** Utafiti wa Sauti za Wananchi, Awamu ya 18 (Aprili 2017)

Chadema inakubalika zaidi miongoni mwa wanaume, vijana, matajiri na wenye kiwango kikubwa cha elimu. Lakini pale CCM inapoungwa mkono kwa kiwango kidogo haimaanishi moja kwa moja kuwa Chadema inaungwa mkono kwa kiwango kikubwa, hasa katika maeneo ya mijini na miongoni mwa wasomi. Hata hivyo, miongoni mwa makundi hayo, wananchi wasiofungamana na chama chochote ni wengi kuliko wale walio karibu na Chadema (haimo kwenye jedwali).

## 3. Hitimisho

Muhtasari huu unaonesha ushahidi unaounga mkono mtiririko wa matukio chini ya utawala wa Rais Magufuli kwa kuainisha mambo chanya pamoja na changamoto kadhaa.

Kwa upande mmoja, tatizo la rushwa limeshuka katika orodha ya kero kubwa za wananchi. Chanzo kinaweza kuwa ni msimamo mkali wa serikali ya awamu ya tano dhidi ya rushwa. Wananchi pia wanataja afya, elimu na maji kama matatizo ambayo si makubwa sana ikilinganishwa na miaka iliyopita. Inawezekana kwamba wananchi wanapokea juhudi zinazofanywa na serikali katika sekta hizi.

Wakati huo huo, wananchi wametaja tatizo la upungufu wa chakula kuwa ni kubwa sana, kuliko ilivyokuwa miaka iliyopita. Matokeo haya yanaunga mkono matokeo yaliyopatikana na utafiti wa *Sauti za Wananchi* wa mwezi Februari 2017, ambapo wananchi nane kati ya kumi walisema kuna upungufu wa chakula kwenye maeneo yao[4].

Kushuka kwa asilimia 25 ya kukubalika kwa utendaji wa Rais kunamaanisha nini? Je kuna uwiano gani kati ya jambo hili na matatizo ya upungufu wa chakula na hali ngumu ya uchumi yaliyotajwa na wananchi? Je, ukosoaji unaofanywa na vyama vya siasa na watu wengine kuwa Rais hatoi uzito wa kutosha katika masuala ya kidemokrasia na haki za binadamu umechangia?

Muhtasari huu unaonesha dalili za wananchi kubadilisha matarajio yao. Kiwango kikubwa cha kukubalika kwa Rais mwaka 2016 (asilimia 96)[5] kimeshuka ghafla. Ujumbe wa wananchi ni kwamba wanajihisi wameangushwa na utendaji wa serikali katika kushughulikia shida zao za msingi: uhakika wa kipato na kula. Ni ishara ya kupungua kwa matumaini waliokuwa nayo mwanzoni. Hata hivyo, hawajavutiwa na chama kingine chochote. Wanasiasa wote wanaambiwa kwamba siasa itumike kuwanufaisha wananchi moja kwa moja kwa kuelewa shida zao na kuzitatua kikamilifu.

---

4 Sauti za Wananchi – *Hunger pangs: Food (in) security in Tanzania*, February 2017. Angalia http://www.twaweza.org/index.php?i=1506.

5 Sauti za Wananchi – The People's President? Citizens' assessment and expectations of the fifth phase government, September 2016. Angalia http://www.twaweza.org/go/sauti-government-performance-2016